


JE! MSITU WA HIFADHI WA KIJIKI CHAKO UMETANGAZWA KWENYE GAZETI LA SERIKALI?

Kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14, 2002 kifungu cha 32 (1); Serikali ya Kijiji itakuwa na uhalali wa kumiliki Msitu wa Hifadhi katika Ardhi ya Kijiji endapo msitu huo:

- Utakuwa umetangazwa na kusajiliwa kwenye daftari la halmashauri husika; na/au
- Utakuwa umetangazwa kwenye Gazeti la Serikali (GN);

Kwa kuzingatia Kifungu namba 35 (1) cha Sheria ya Misitu Na. 14 ya 2002, Serikali ya Kijiji ikishasimamia Msitu wa Hifadhi wa Kijiji uliotangazwa na kusajiliwa kwenye daftari la Halmashauri ya Wilaya husika, kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (3); inaweza kupeleka Maombi ya Kutangaza Msitu huo kwenye Gazeti la Serikali. Maombi yatapelekwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya.



Hatua za Kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Kijiji kwenye Gazeti la Serikali

Hatua ya 1:

Kijiji kitaanda maombi yenye viambatanisho vifuatavyo, kumwomba Mkurugenzi wa idara ya Misitu na Nyuki kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Kijiji kwenye gazeti la Serikali.

- Muhtasari wa mkutano mkuu wa kijiji ulioazimia kuanzishwa kwa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji;
- Majina ya Wajumbe wa Kamati ya Maliasili au chombo kingine kilichowekwa kwa mujibu wa vifungu namba 33 (1) (d), (2) na 34 (3) vya Sheria Ya Misitu Na. 14, 2002;
- Ramani Rasmi au ushahidi wa kimaandishi unaonesha mipaka ya Ardhi ya Kijiji; Msitu wa Hifadhi wa Kijiji na Vijiji Jirani vinavyopakana nao;
- Nakala ya mpango wa Usimamizi wa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji;
- Nakala rasmi ya Sheria ndogo ya Usimamizi wa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji;
- Maelezo mafupi ya sababu ya kijiji kuomba kutangaza msitu wake kwenye gazeti la Serikali na madhumuni ya kuanzisha Msitu huo kuwa Hifadhi ya Kijiji;
- Maelezo mafupi kuhusu utaratibu wa usimamizi wa fedha zitokanazo na Msitu wa Hifadhi wa Kijiji;
- Maelezo mafupi ya watumishi walioajiriwa na halmashauri ya kijiji ili kusimamia msitu wa hifadhi wa kijiji (Kama wapo).

Hatua ya 2:

Serikali ya Kijiji itapeleka maombi kwa Mkurugenzi wa halmashauri ya husika, ambaye atayahakiki na kutoa taarifa ya matokeo ya uhakiki huo ndani ya kipindi cha siku 60 tangu tarehe ya kupokea maombi hayo kutoka kijijini.

Hatua ya 3:

Endapo Maombi ya Kijiji yatakuwa hayana dosari yoyote Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika atayawasilisha kwa Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki kwa niaba ya Serikali ya kijiji.

Hatua ya 4:

Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, ataamua ama kukubali maombi ya kijiji bila masharti au kwa masharti na atatoa sababu za masharti hayo, na kama atakataa maombi pia atatoa sababu.

Hatua ya 5:

- Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki
- ataitaarifu halmashauri ya kijiji husika matokeo ya maombi yao;
 - kama maombi yamekidhi vigezo vyote atautangaza Msitu wa Hifadhi wa Kijiji kwenye **GAZETI LA SERIKALI (GN)**.

Faida za kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Kijiji Kwenye Gazeti la Serikali

- Kurasimisha zaidi Msitu wa Hifadhi wa Kijiji na kuufanya ujulikane zaidi kitaifa na kimataifa
- Kuupa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji hadhi ya juu na kuufanya uheshimike zaidi kisheria



Kwa mawasiliano zaidi: Wizara ya Maliasili na Utalii, Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, Mji wa Serikali, Mtumba, S.L.P. 1531, Dodoma